

TANZANIA / JUDGMENT

MAOMBI YA MAREJEO NA 277 OF 2023 JUMA MOSHI LUGELO VRS TAN CHOICE LTD

COURT
TANZLIIDECIDED
1 January 2023

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DIVISHENI YA KAZI ILIYOKETI DAR ES SALAAM MAOMBI YA MAREJEO NA. 277 YA 2023 (Marejeo yanatokana na uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ya PWN iliyoketi Kibaha, Tarehe 14 Septemba 2023 katika Mgogoro wa Kazi Na. CM A/PW N/KBH/87/2022/28/2022) BAIN A YA JUMA MOSHI LUGELO.....MLETA MAOMBI N A .I IKIWANI UDODO HASSAN..... MLETA MAOMBI NA.2 NA TAN CHOICE LTD..... MJIBU MAOMBI HUKUMU Tarehe ya mwisho ya Amri; 4/4/2024 Tarehe ya Hukumu: 31/5/2024 OPIYQ. J. Marejeo haya yanatokana na uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Mgogoro wa Kazi Na. CMA/PWN/KBH/87/2022/28/2022. ju m a m o s h i l u g e l o n a m w e n z a k e a m b a o n i w a l e t a m a o m b i w a n a o m b a M a h a k a m a h i i i i p i t i e n a k u t e n g u a , n a m a r a b a a d a y a k u t e n g u a i m u a m u r u m j i b u m a o m b i k u w a l i p a w a l e t a m a o m b i f i d i a i s i y o p u n g u a k i a s i c h a f e d h a T s h 5 , 0 2 3 , 5 3 7 / = n a k u t o a n a f u u n y i n g i n e y o y o t e a m b a y o w a l e t a m a o m b i w a n a s t a h i l i k u p a t a . H i s t o r i a f u p i y a s h a u r i h i l i n i k w a m b a w a l e t a m a o m b i w a l i a j i r i w a k w a n y a k a t i t o f a u t i k w a k u f a n y a k a z i y a k u c h i n j a n a k u t u n z a w a n y a m a a l i a j i r i w a k w a m k a t a b a w a m w a k a m m o j a . M a h u s i a n o y a k i a j i r a y a l i k o m a t a r e h e 2 3 / 1 1 / 2 0 2 3 b a a d a y a m w a j i r i / m j i b u m a o m b i k u s i t i s h a a j i r a y a w a l e t a m a o m b i k w a m a d a i y a u t o v u w a n i d h a m u u n a o t o k a n a n a u t o r o k a z i n i . W a l e t a M a o m b i h a w a k u r i d h i k a n a m a a u m u z i h a y o , h i v y o k u p e l e k e a k u f u n g u l i w a k w a m g o g o r o w a k a z i m b e l e y a T u m e . H a t a h i v y o T u m e i l i t u p i l i a m b a l i m a d a i y a w a l e t a m a o m b i k w a k u o n a u a c h i s h w a j i k a z i u l i k u w a w a h a k i n a k i s h e r i a , h i v y o k u p e l e k e a k u f u n g u l i w a k w a m a o m b i h a y a . M a o m b i h a y a , y a l i a m b a t a n a n a k i a p o c h a P a m o j a c h a w a l e t a m a o m b i , a m b a c h o k i k i e l e z e a m t r i r i k o m z i m a w a m g o g o r o h u u u l i o p e l e k e a m a o m b i h a y a k a m a i l i v y o e l e z w a h a p o j u u , a m b a p o w a l e t a m a o m b i w a n a d a i m u a m u z i a l i k o s e a k i m a n t i k i n a k i s h e r i a k w a k u a m u a k w a m b a m j i b u m a o m b i a l i k u w a n a s a b a b u z a m s i n g i z a k u w a a c h i s h a k a z i , k w a k u t u m i a k u m b u k u m b u z a n y u m a a m b a z o h a z i k u w a h i k u f a n y i w a u c h u n g u z i . S h a u r i h i l i l i l i s i k i l i z w a k w a n j i a y a m a a n d i s h i , a m b a p o w a l e t a M a o m b i w a l i w a k i l i s h w a n a B w . E d w a r d S i m k o k o , M w a k i l i s h i B i n a f s i . W a k a t i m j i b u m a o m b i a l i w a k i l i s h w a n a B w . C e a s o r K a b i s a , w a k i l i . M a h a k a m a h i i i m e z i n g a t i a m a w a s i l i s h o y a p a n d e z o t e m b i l i , a m b a y o y a t a t u m i k a k a t i k a u a m u z i h u u . H a t a h i v y o h o j a b i s h a n i w a k a t i k a s h a u r i h i l i n i j e p a l i k u w a p o n a s a b a b u y a m s i n g i y a u a c h i s h w a j i k a z i

inayoendana na adhabu ya uachishwaji kazi na je mjibu maombi alikuwa sahihi kuwaachisha kazi waleta maombi kwa kutumia kumbukumbu za nyuma ambazo hazikufanyiwa utafiti. Kuhusu hoja ya kwanza ya kwamba je palikuwapo na sababu ya msingi ya uachishwaji kazi inayoendana na adhabu ya uachishwaji kazi, Bw. Simkoko alieleza kwamba hapakuwepo na sababu ya msingi ya kuwaachisha kazi waleta maombi kwa kutohudhuria kazini kwa muda wa siku mbili, alieleza ya kwamba maamuzi ya mjibu maombi yanaenda kinyume na msimamo wa sheria ikiwepo Kanuni ya 12 ya T.S Na.42 la 2007 inayomtaka muamuzi katika makosa ya nidhamu kuzingatia adhabu mbadala na siyo kuachisha kazi. Katika kuipa nguvu hoja yake alirejea kesi Constantine Victor John v. Muhimbili National Hospital, Maombi ya Madai Na.188/01 ya 2021 na kesi ya Sunder Chemical Fiber Limited v. Judith Thadey Mrosso, Marejeo Na.432 ya 2023 ambazo zimetoa msimamo ya kwamba kutofika kazini kwa siku zisizozidi (5) tano, siyo sababu ya msingi kumwachisha mfanyakazi kazi. Kwa upande wa mjibu maombi alieleza ya kwamba muamuzi alikuwa sahihi kwa kuamua ya kwamba palikuwepo na sababu ya msingi ya uachishwaji kazi kutokana na ushahidi uliotolewa, kwani waleta maombi walikuwa na mazoea ya utoro kazini jam bo lililopelekea kuathiri shughuli za utendeji na hasara kwani mjibu maombi kuna wakati ilibidi awaajiri vibarua wa muda ili wafanye kazi za waleta maombi. Aliendelea kwa kueleza ya kwamba kutokana na uasili wa kazi ya mwajiri waleta maombi hawakutakiwa kuwa watoro kazini. Katika kutilia mkazo hoja yake alirejea kesi ya Bulyamhulu Gold Mine Ltd v. George Allen Gwabo, Marejeo Na. 48 ya 2015, Mahakama kuu, Divisheni ya Kazi ambayo ilitoa msimamo wa kisheria ya kwamba utoro uliokithiri japokuwa sio mfulilizo ni sababu tosha ya kumwachisha mwajiriwa kazi. Katika kujibu hoja ya uwepo wa sababu ya uachishwaji kazi ni wazi ya kwamba kwa mujibu wa K/F cha 39 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, Sura ya 366 Marekebisho ya 2019, kinamtaka mwajiri kuthibitisha uhalali wa uachishwaji kazi. Katika shauri hili kielelezo D9 (rejista ya mahudhurio) inaonyesha baadhi ya siku ambazo waleta maombi hawakufika kazini pasipokuwa na kibali cha ruhusa. Pia hakuna ubishi ya kwamba ni mara nyingi waleta maombi wamekuwa hawafiki Hata hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 12(4)(b) T.S Na. 42 la 2007 ni wazi inatamka kwamba katika kuamua kama uachishwaji kazi ni adhabu sahihi, mwajili ataangaiia vitu vingi ikiwepo taarifa za nyuma za mwajiriwa, jam bo ambao imejidhihiisha katika shauri hili ambapo Kielelezo D7(onyo la mdomo) na D8 (onyo la maandishi) vinaonyesha waleta maombi, kila mmoja ameonywa zaidi ya mara moja juu ya tabia ya utoro na hivyo kwa mtizamo wa Mahakama hii inaona ni utoro uliokithiri, hivyo kuikubali hoja ya mjibu maombi kama ilivyojadiliwa katika Kesi tajwa hapo juu, kesi ya Buiyamhulu Gold Mine Ltd v. George Allen Gwabo, Marejeo Na. 48 ya 2015, Mahakama kuu, Divisheni ya Kazi ambayo ilitoa msimamo wa kisheria ya kwamba utoro uliokithiri japokuwa sio mfulilizo ni sababu tosha ya kumwachisha mwajiriwa kazi. Kutokana na msimamo wa kisheria hapo juu ni wazi ya kwamba muamuzi wa tume alikuwa sahihi si tu kwa kuamua ya kwamba palikuwapo na sababu ya msingi bali adhabu ya uachishwaji kazi ilikuwa sahihi, kwa sababu waleta maombi walikwishaipata nafuu nyingine baada ya mwajiri kuwapa onyo mara kwa mara pasipokuwepo mabadiliko. Katika msimamo huu hoja ya pili ya waleta maombi kwamba hapakuwa na uchunguzi inakosa mashiko kwani hakuna ubishi ya kwamba wamekuwa na tabia ya kutofika kazini kulingana na rejista ya mahudhurio katika kielelezo D9. Katika mazingira haya nayakataa maombi haya ya Marejeo kwa kuwa hayana mashiko kisheria, na kushikilia maamuzi ya Tume. Kila upande Utabeba gharama zake katika

shauli hili. Amri hii irnetolewa leo.

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE	https://media.tanzlii.org/media/judgment/316056/source_file/a5ca5a6de55c0dc7/MAOMBI_YA_MAREJEO_NA_277_OF_2023__JUMA_MOSHI_LUGELO_VRS__TAN_CHOICE_LTD.pdf
CASE PAGE	https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/juma-moshi-lugelo-v-tan-choice-ltd-unfairtermination-tanzlii-2023--6a3ea52c3b1caa9129825921

Prepared on 14 October 2026 · Esheria